

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS**  
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**MKOA WA DAR ES SALAAM**

Anwani ya Simu:  
Simu: 2203156/58  
Fax: +25522203213  
Tovuti: [www.dsm.go.tz](http://www.dsm.go.tz)  
Barua Pepe: [ras@dsm.go.tz](mailto:ras@dsm.go.tz)



**OFISI YA MKUU WA MKOA**  
**3 Barabara ya Rashidi**  
**Kawawa,**  
S.L.P 5429,  
**12880 -DAR ES SALAAM.**  
**Tanzania**

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

Rais wa Makampuni ya **CNBM** kutoka Beijing CHINA Bw. Cao Jiang Lin amekutana na kufanya mazungumzo na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Paul C. Makonda, Jijini Dar es Salaam.

Katika mazungumzo hayo, Bw. Lin amemuhakikishia Mkuu wa Mkoa Mhe. Makonda kuwa Makampuni mengi yameonyesha nia ya dhati ya kuja kuwekeza nchini Tanzania ambapo tayari baadhi ya Makampuni yameshaanza kuwekeza Jijini **Dar es Salaam**.

Aidha, katika mazungumzo yao, Bw. Lin amemuahidi Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Mhe. Paul C. Makonda **kuwapatia kazi vijana wa Dar es Salaam Zaidi ya 500 kupitia Ofisi ya Mkuu wa Mkoa**.

Ikumbukwe kuwa Makampuni ya **CNBM** yako Zaidi ya **500 duniani** na ndiyo Makampuni yanayoongoza kwa uzalishaji wa Cement na bidhaa Zaidi ya **15,000 DUNIANI**.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhusiano

**OFISI YA MKUU WA MKOA**

**DAR ES SALAAM**

28/05/2017